## 5.0 GHARAMA KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI

Serikali hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati pale wanapoomba bidhaa zao wanazozizalisha wenyewe zithibitishwe ubora. Kati yao wapo ambao wanasamehewa kulipa ada yoyote kwa sababu ya mitaji yao kuwa midogo.

**Ili kupata msamaha huu, mjasiriamali anatakiwa:**

- Kupata barua ya utambulisho kutoka ofisi ya sido
- Kuwa na leseni ya biashara.

Wajasiriamali waliokwishapata leseni ya kutumia alama ya ubora wanapaswa kutunza taarifa za uzalishaji na mauzo ambazo watatakiwa kuzionesha kwa wakaguzi wa TBS pindi zinapohitajika.

**Kwa maelezo zaidi,wasiliana nasi kwa anwani zifuatazo:**


### MKURUGENZI MKUU

Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
S.L.P. 9524, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2450298 / 2450206/2451763-6
Hotline: +0800 110 827/ Nukushi: + 255 22 2450959
Baruapepe: info@tbs.go.tz/ Tovuti: www.tbs.go.tz
Malalamiko: malalamiko@tbs.go.tz

**OFISI ZA KANDA:**

**NYANDA ZA JUU KUSINI**
(Iringa, Mbeya, Njombe and Songwe)
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S.L.P. 1674 Mbeya, Tanzania
Simu: 025 2502848 / Nukushi: 025 2502848

**KANDA YA ZIWA**
(Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu and Shiyanga)
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S.L.P. 1814 Mwanza, Tanzania
Simu: 028 2505044 / Nukushi: 028 2505044

**KANDA YA KASKAZINI**
(Arusha, Kilimanjaro, Manyara and Tanga)
Ngorongoro Tourist Center, Ghorofa ya 6
S.L.P. 2399 Arusha, Tanzania
Simu: 027 2520143 / Nukushi: 027 2520143

**KANDA YA KATI**
(Dodoma, Singida and Tabora)
Kambarage Tower, Ghorofa ya 6
S.L.P 2956, Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2320310 / Nukushi: 026 2320310

**KANDA YA KUSINI**
(Lindi, Mtwara and Ruvuma)
Jengo la PSSSF, Sokoine House, Ghorofa ya 3
S.L.P 1396 Mtwara,Tanzania
Simu: 023 2334477 / Nukushi: 023 2334477

**KANDA YA MAGHARIBI**
(Katavi, Kigoma and Rukwa)
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S.L.P 1276 Kigoma,Tanzania
Simu: 028 2804023 / Nukushi: 028 2804023

TBS_Tanzania  tbs_viwango  TBS Viwango TV


TANZANIA BUREAU OF STANDARDS

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)

# UTARATIBU WA KUPATA ALAMA YA UBORA

## 1.0 TBS KWA UFUPI

### 1.1 Utangulizi

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge – Sheria ya Viwango Na. 3 ya mwaka 1975, iliyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 1 ya mwaka 1977. Sheria hiyo ilifutwa na nafasi yake kuchukuliwa na Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 ambayo ililipa Shirika uwezo mkubwa zaidi wa kutekeleza majukumu yake.

### 1.2 Dhima

Dhima ya Shirika ni kueneza uelewa na kukuza matumizi ya viwango na udhibiti ubora katika viwanda, biashara na huduma, kwa lengo la kuchangia katika juhudi za kitaifa za kuzalisha bidhaa na huduma bora zenye uwezo wa kushindana katika soko la ndani na la kimataifa, hivyo kuchochea maendeleo ya uchumi.

### 1.3 Majukumu ya Shirika

Shirika lina majukumu mengi kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009, lakini majukumu makuu manne ni:

a) Kuweka viwango vya kitaifa vya bidhaa, huduma na mifumo ya usimamizi wa ubora katika sekta zote;

b) Kutekeleza viwango vya kitaifa katika sekta za viwanda, biashara na huduma, kwa kutumia skimu mbalimbali za udhibiti ubora;

c) Upimaji wa bidhaa kwa lengo la kuhakikisha ubora wake, pamoja na ugezi wa zana za kupimia viwandani; na

d) Kutoa mafunzo kwa wazalishaji pamoja na wafanyakazi katika taasisi na viwanda kuhusiana uzalishaji wa bidhaa bora, uzalishaji salama na usimamizi wa ubora.

## 2.0 UDHIBITI WA UBORA

TBS inazo skimu mbalimbali za udhibiti ubora. Mojawapo ya skimu hizo ni Skimu ya Alama ya Ubora. Chini ya skimu hii, mzalishaji ambaye bidhaa yake imethibitishwa ubora kwa kuzingatia kiwango cha kitaifa cha bidhaa husika hupewa leseni ya kutumia alama ya TBS katika bidhaa hiyo.

Alama ya ubora ya TBS ikiwa kwenye bidhaa huonyesha kuwa bidhaa husika imepimwa na kuthibitishwa ubora wake na TBS kwa kuzingatia matakwa ya kiwango cha bidhaa husika. Alama hiyo ni uthibitisho kwa mzalishaji na mlaji kuwa bidhaa husika ni bora na salama kwa matumizi na kwa mazingira.

Alama ya ubora ya TBS huwafanya wanunuzi kununua bidhaa bila wasiwasi wowote. Kwa upande mwingine alama hiyo humlinda mzalishaji katika ushindani dhidi ya bidhaa hafifu na humwezesha kulihakikishia soko lake kuwa bidhaa yake inakidhi matakwa yaliyobainishwa katika kiwango na hivyo ni bora na salama kwa matumizi yaliyokusudiwa.

## 3.0 UTARATIBU WA KUPATA ALAMA YA UBORA

### 3.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Maombi ya kupata alama ya ubora wa bidhaa hufanywa na muombaji kupitia mfumo wa kielektroniki (i-SQMT) unapatikana kupitia tovuti ya TBS (www.tbs.go.tz) kwenye kitufe cha e-SERVICE au moja kwa moja kupitia linki ya https://portal.tbs.go.tz

Baada ya maombi kukamilika tarehe ya ukaguzi wa awali hupangwa. izingatiwe kuwa mwenye kiwanda anatakiwa kuwa katika uzalishaji siku ya kufanya ukaguzi wa awali

### 3.2 Hatua ya Pili – Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali hufanywa na wakaguzi wa TBS. Sampuli huchukuliwa na kupimwa ili kuona kama bidhaa inakidhi matakwa ya kiwango husika. Mkaguzi huandaa taarifa kuhusu hali halisi ya kiwanda na mambo yanayostahili kurekebishwa.

### 3.3 Hatua ya Tatu – Upimaji

Sampuli zilizochukuliwa hupimwa katika maabara za TBS kwa kufuata kiwango husika. Baada ya kazi ya upimaji kumalizika, ripoti hutolewa kwa mwombaji.

### 3.4 Hatua ya Nne – Utoaji wa Leseni

Uamuzi kuhusu kutoa au kutotoa leseni ya kutumia alama ya ubora hutegemea tu ripoti ya ukaguzi wa awali wa kiwanda pamoja na ripoti ya maabara. Kimsingi ripoti zote mbili zinatakiwa kuonyesha kwamba mazingira ya uzalishaji kiwandani, mfumo wa uzalishaji na bidhaa iliyopimwa havina matatizo.

Ikiwa sivyo basi mzalishaji hutakiwa kufanya marekebisho na baadaye mkaguzi wa TBS hutumwa tena na kuleta sampuli nyingine.

## 4.0 MUDA WA LESENI YA ALAMA YA UBORA

Leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS hudumu kwa mwaka mmoja na huhuishwa baada ya kuhakikisha kwamba taratibu zilizokubalika zinafuatwa.